**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**


***Simu Na.*** **255-252957128**
***Nukushi:*** **255-25295712,**
**Manispaa,**
**Barua pepe:** ***md@mpandamc.go.tz***

**Ofisi ya Mkurugenzi**
**Halmashauri ya**
**S.L.P. 216,**
**MPANDA.**


# TANGAZO

---

## ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA USAFI HOSPITALI YA HALMASHAURI YA MANISPAA KWA KIPINDI CHA JULAI 2018 HADI JUNI 2019

## ZABUNI No:LGA.101/2018/2019/CQ/NC/04

**Tarehe: 30/05/2018**

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda inakaribisha maombi ya Zabuni kutoka kwenye Taasisi /Mashirika/Makampuni na watu binafsi wenye uwezo, leseni, uzoefu na sifa za kutoa huduma ya Usafi kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kwa kipindi cha kuanzia Julai 01, 2018 hadi Juni 31, 2019.  Zabuni ya kutoa Huduma ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwari hapo chini:-

| S/N | NAMBA YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI |
|---|---|---|
| 1. | LGA.101/2018/2019/CQ/NC/04 | Zabuni ya Huduma ya usafi wa Hospitali a Manispaa maeneo yote yanayo zunguka Hospitali, Maeneo ya Ndani na nje ya majengo ya Hospitali ya Manispaa. |

2. Maombi yote ya Nukuu za Bei yazingatie masharti yafuatayo:-

i) Nyaraka za Nukuu za bei zitapatikana mara baada ya Mwombaji kutembelea eneo la biashara kabla ya kuchukua nyaraka ya zabuni ambayo itatolewa baada ya kutembelea eneo la biashara.

ii) Ombi la Nukuu za bei liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (physical address)

iii) Mwombaji awe na ofisi inayojulikana mahali ilipo na itambulike kisheria.

iv) Zingatia kuwa fomu ya maombi ya Nukuu za bei inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney) katika zabuni hii.

3. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote tofauti na yanayo husu Nukuu ya bei (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, Original au Copy, Anuani ya Katibu wa Bodi ya zabuni, S.L.P 216, Mpanda-Katavi bila kuwekwa alama yoyote.

4. Mwisho wa kupokea Nukuu za bei ni saa nne (4) kamili asubuhi (saa za Afrika Mashariki) ya tarehe 05 Mwezi June, 2018 katika ofisi za Halmashauri ya Manispaa, Kitengo cha Ununuzi (PMU) S.L.P 216, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda katika ofisi mpya za makao

mapya zilizopo Ilembo. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo katika ukumbi wa Halmashauri

5. Anuani ya kutuma zabuni hizo ni kwa: Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, S.L.P 216, **MPANDA-KATAVI**

6. Barua zote za maombi zipitishwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kupata usajili kabla ya kudumbukizwa kwenye sanduku la Zabuni na maombi yatumbukizwe katika sanduku la Zabuni lililopo kwenye jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa - Mpanda.

7. Tangazo hili ni la **siku 7** tangu tarehe **30/05/2018 hadi 05/06/2018** majira ya Saa **Nne asubuhi**.

8. Kwa Zabuni hii ya kutoa huduma mbalimbali za Halmashauri ya Manispaa muda wake ni kipindi cha mwaka mmoja yaani kuanzia Julai 1, 2018 hadi Juni 30, 2019.

9. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa, Sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielekitroniki (e-mail), Zabuni ambazo hazitapokelewa, Zabuni ambazo hazitafunguliwa na kusomwa hadharani katika tukio la Ufunguzi wa Zabuni hazitakubalika kufanyiwa tathmini katika hali yoyote ile.

Michael F. Nzyungu
Mkurugenzi wa Manispaa
**MPANDA-KATAVI**